MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

**Na. 2 Toleo Maalum: Utabiri wa msimu wa mvua za Novemba hadi Aprili ( *NDJFMA )*, 2019 Limetolewa tarehe, 10 Octoba, 2019**

**MUHTASARI**

- Msimu wa mvua wa Novemba hadi April(NDJFMA) ni mahusus kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka
- Kiwango cha mvua za kutosha kinatarajiwa kuongezeka katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu wa mvua NDJFMA 2019/2020.
- Mvua za msimu zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani kwa maeneo mengi ya nchi.
- Malisho na maji ya mifugo vinatarajiwa kuongezeka hivyo kupelekea kupngua kwa migororo ya wakulima na wafugaji.

## MWELEKEO WA MIFUMO YA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA NOVEMBA HADI APRILI, 2019/2020

Katika bahari ya Hindi, eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la juu zaidi ya wastani kulinganisha na eneo la mashariki mwa bahari hiyo (Pwani ya Indonesia). Hata hivyo, joto la juu zaidi linaonekana katika eneo la kati ya bahari ya Hindi na Pwani ya Somalia. Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani hali inayotarajiwa kusababisha kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa na vimbunga katika eneo hilo.

Migandamizo midogo ya hewa pamoja na vimbunga katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi inatarajiwa kuvuta upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo na hivyo kusababisha mvua katika maeneo mengi hapa nchini.

Katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki, joto la bahari linatarajiwa kuwa la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango mdogo kwa mifumo na mwenendo wa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## MWELEKEO WA MVUA ZA *MSIMU (NDJFMA)* 2019/2020

Mvua za *Msimu* ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa ,mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka maeneo machache hususan mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Hata hivyo, mvua nyingi zinatarajiwa kunyesha katika nusu ya kwanza ya msimu, kutokana na uwezekano wa uwepo wa upepo kuvuma kutoka magharibi. Upepo huu unatarajiwa kubeba unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea katika maeneo ya nchi yetu. Kipindi cha nusu ya pili cha msimu, mvua zinatarajiwa kupungua katika baadhi ya maeneo kutokana na joto la bahari sehemu ya kati ya bahari ya Hindi kuendelea kuongezeka ikilinganishwa na maeneo mengine ya bahari ya Hindi. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

**Kanda ya Magharibi: (Mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi)**
Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika mkoa wa Tabora. Aidha, mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma na Katavi. Mvua hizi zinatarajiwa kuanza katika wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2019 katika mkoa wa Kigoma na kusambaa katika mikoa ya Katavi na Tabora katika wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2019. Mvua hizo zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2020.


**Kanda ya Kati: (Mikoa ya Singida na Dodoma)**
Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza hadi wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2019. Maeneo haya yanatarajiwa kupata mvua za juu ya wastani hadi wastani. Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya pili na wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2020.

**Nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya kusini mwa nchi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro)**

Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya kwanza na wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2019 na zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi. Hata hivyo, katika maeneo machache ya magharibi mwa mkoa wa Ruvuma mvua zinatarajiwa kuwa za wastani. Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2020 na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2020.

**Pwani ya kusini: (Mikoa ya Lindi na Mtwara)**

Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya kwanza na wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2019 na zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi. Mvua zinatarajiwa kuisha katika wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2020.




Kielelezo: Mwelekeo wa mvua za ***Novemba hadi Aprili 2019/*** *2020*

## ATHARI NA USHAURI

**Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Wanyamapori**

Katika kipindi cha mvua za '*Msimu'* hali ya unyevunyevu wa udongo kwa ustawi wa mazao vinatarajiwa kuimarika katika maeneo mengi. Mazao yasiyohitaji maji mengi, kama vile mahindi, maharage na mtama,yanaweza kuathiriwa na hali ya unyevunyevu wa kupitiliza na maji kutuama mashambani hususan kwa maeneo yanayotarajiwa kuwa na mvua za juu ya wastani hadi wastani. Magonjwa ya wanyama na uharibifu wa miundombinu ya kilimo vinaweza kujitokeza kutokana na mvua zinazotarajiwa. Upatikanaji wa chakula cha samaki unatarajiwa kuongezeka kutokana na mvua za msimu za juu ya wastani hadi wastani zinazotarajiwa. Hali hii itasaidia kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya Uvuvi. Wadau katika sekta ya uvuvi wanashauriwa kuandaa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya Uvuvi yakiwemo maghala ya baridi. Inashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki hasa kwenye mabwawa kutokana na uwezekano wa kuwepo mvua kubwa. Malisho na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na wanyama pori vinatarajiwa kuwa vya kuridhisha katika maeneo mengi. Teknolojia ya uvunaji maji ya mvua iimarishwe ili kuhifadhi maji kwa matumizi katika kipindi cha baadae. Pamoja na ushauri huu watumiaji wa taarifa za hali ya hewa wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa wataalam wa sekta husika ikiwemo maafisa ugani.

**Maji**

Upatikanaji wa maji unatarajiwa kuimarika, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za juu ya wastani hadi wastani. Kina cha maji katika mabwawa na mito kinatarajiwa kuongezeka.Wakulima na wafugaji wanashauri kutumia maji kwa uangalifu na kutumia mbinu bora za kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

**Menejimenti ya Maafa**

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za juu ya wastani hadi wastani, inashauriwa taarifa zitolewe kwa wakazi wa maeneo ya mabondeni, karibu na mito, na yale ya tambarare, kupitia ngazi zinazohusika kama vile Kamati za maafa za Mkoa na Wilaya. Kamati zinashauriwa kufanya maandalizi ikiwemo kutafuta na kutenga rasilimali za kukabiliana na maafa yanayoweza kujitokeza. Aidha, taasisi, kampuni za ujenzi na usafirishaji pamoja na wadau wengine wanashauriwa kujiandaa kuchukua hatua za dharura iwapo kutatokea uharibifu wa miundombinu ili kupunguza athari na hasara zinazoweza kutokea. Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani, wananchi na wadau wengine wanashauriwa kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii kama kawaida.

***Zingatio: Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia tabiri za saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari za hali mbaya ya hewa kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.***

*Jarida limetayarishwa na:*
**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**
**Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro,** Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8;***
***Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***